TANGAZO LA SERIKALI Na. 43 la tarehe. 24/1/2024

# SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI), (SURA YA 288)

## SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2025

Jina

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"kaya" maana yake ni baba, mama na watoto wenye umri usiozidi miaka kumi na nane au mtu yeyote aliyetimiza umri wa kuanzia miaka kumi na nane awe na mtoto au bila mtoto;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote kinachosababisha-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya ya kuudhi;
(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari au viumbe wengine hatari;
(d) magonjwa kwa binadamu;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi na inajumuisha maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri, taasisi ya umma au mtu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

"meneja wa machinjio" maana yake ni kiongozi wa machinjio yanayomilikiwa na Halmashauri aliyeteuliwa kwa mujibu wa Hati ya Uanzishaji wa Bodi ya Huduma ya Machinjio ya Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, nguruwe na wanyama wengine wanaofugwa na binadamu;

"mkaguzi wa nyama" maana yake ni mtaalamu wa afya ya mifugo aliyeajiriwa na Serikali na kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa na Baraza la Vetenari Tanzania;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki wa machinjio" maana yake ni mtu yeyote au taasisi inayomiliki machinjio binafsi katika eneo la Halmashauri;

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo wa kulishia mifugo ndani ya jengo lililoruhusiwa;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi, shirika au kampuni iliyoteuliwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Halmashauri

**4.** Katika kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa mifugo, Halmshauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji anaruhusiwa kufuga kulingana na ukubwa wa eneo lake;

(c) kuanzisha na kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;

(d) kutoa elimu ya ufugaji bora ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo yao kwa kuuza wanyama hai au kwa kuchinja na kuuza nyama ili kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kutoa huduma za chanjo kwa kushirikiana na wafugaji ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza kwa binadamu; na
(g) kudhibiti uzururaji wa mifugo na wanyama katika Halmashauri.

Wajibu wa mfugaji

**5.** Ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo, kila mfugaji atahakikisha kuwa-
(a) anafuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi
(b) anafanya ufugaji wa ndani kulingana na maelekezo yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii;
(c) mifugo inapata malisho, chakula na maji kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;
(d) anahudhuria mafunzo ya ufugaji bora;
(e) anadhibiti magonjwa ya wanyama kwa kuogesha na kuipatia chanjo mifugo
(f) mifugo inawekewa alama maalumu kwa ajili ya utambuzi kwa kuzingatia Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Wanyama; (Sura ya 184)
(g) anakuwa na kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(h) ana kibali cha kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo;
(i) anauza mifugo katika masoko na minada iliyoidhinishwa au eneo lingine kwa taarifa maalum.

Kibali cha kufuga mifugo mjini

**6.-**(1) Mtu yeyote anayekusudia kufuga mifugo atapaswa atapaswa kuomba kibali cha kufuga kutoka kwa Halmashauri.

(2) Kibali cha ufugaji hakitakuwa na gharama na kitakuwa cha miaka mitatu kuanzia tarehe kilipotolewa.

(3) Kibali cha ufugaji kitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(4) Halmashauri inaweza kufuta kibali cha mtu yeyote atakayekiuka taratibu za ufugaji zilizoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Masharti ya kufuga mjini

**7.** Kila mfugaji hataruhusiwa-

(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;

(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa bila kibali maalumu cha Halmashauri; na

(f) kufuga mifugo zaidi ya idadi iliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Kibali cha kusafirisha mifugo

**8.-**(1) Mtu anayekusudia kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo kwa kuweka utaratibu ikiwa ni pamoja na-

(a) mfugaji kutoa uthibitisho wa kumiliki mifugo kutoka kwa Afisa Mwidhiniwa; na

(b) kukagua kibali cha kusafirisha mifugo.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukamata na kumtoza faini mtu yeyote ambaye atasafirisha mifugo kinyume na Sheria Ndogo hii.

Taratibu za ufugaji

**9.** Mfugaji yeyote atatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

**10.-**(1) Halmashauri itakamata mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) Mifugo itakayokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) italipiwa faini ya shilingi elfu kumi kwa kila siku kwa kila mfugo.

(3) Endapo mifugo iliyokamatwa haitachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuiuza kwa mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mifugo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mifugo, gharama ya mahakama na gharama ya mnada.

(4) Kabla ya kuuza kwa mnada mifugo iliyokamatwa, Halmashauri itatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo.

(5) Endapo mifugo iliyokamatwa itakufa, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama kifo kimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na bidhaa za mifugo

**11.-**(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukataa aina yoyote ya mifugo au mazao ya mifugo kuingia au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba mifugo hiyo au mazao ya mifugo yanaweza kuhatarisha afya au usalama wa mifugo mingine au watumiaji.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kati ya saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri kwa lengo la utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa muda wowote baada ya kupata kibali cha Mkurugenzi.

Taratibu za biashara ya mifugo na

**12.-**(1) Mtu yeyote kabla ya kuanza biashara ya mifugo au mazao ya mifugo atapaswa kuwa na leseni, utambulisho na vibali kutoka Mamlaka husika

mazao ya mifugo

vinavyohusu kuuza na kununua mifugo na mazao ya mifugo na atatakiwa kuwasilisha vibali vyake Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mtu yeyote anayepeleka au kutoa mifugo mnadani au machinjioni atatakiwa kuwa na kibali maalumu kutoka Halmashauri.

(3) Mtu yeyote atakayesafirisha mifugo kutoka nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(4) Mfanyabiashara wa mifugo atapaswa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

(5) Mtu yeyote atapaswa kuuza au kununua mifugo katika minada na masoko yanayotambulika kwa mujibu wa sheria.

(6) Mifugo itakayokamatwa ikisafirishwa bila kibali au kuuzwa eneo ambalo halijaidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo, mhusika atalazimika kulipa faini ya shilingi elfu kumi kwa kila mfugo.

(7) Minada yote ya mifugo au soko la mifugo litafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kwenye maeneo yaliyoruhusiwa.

Wajibu wa mfanyabiashara wa bucha na maduka ya nyama

**13.** Kila mfanyabiashara wa duka la nyama anatakiwa kuhakikisha kuwa-

(a) ana leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;
(b) katika duka lake kuna kabati la vioo la kuzuia inzi na wadudu wengine wataambao na warukao, jokofu la kuhifadhia nyama na pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(c) jengo analotumia kwa ajili ya biashara lina mwanga wa kutosha, umeme, maji safi na salama, visu, meza, mzani wa kawaida au mzani wa kielektroniki, na misumeno maalumu ya kukatia nyama;
(d) nyama imekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na kugongwa muhuri;
(e) muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote ambazo ni mabuti, koti na kofia;

(f) muuzaji anapima afya yake kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji;

(g) mmiliki wa bucha au muuzaji wa nyama anatoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wowote wa ukaguzi; na

(h) biashara ya nyama inafanyika ndani ya bucha au maduka maalumu.

Usafirishaji wa nyama

**14.**-(1) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalum na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki au dereva wa gari la kubeba nyama atahakikisha kuwa gari-

(a) limesajiliwa na kupewa cheti maalumu cha ukaguzi na Halmashauri;

(b) linakaguliwa kila baada ya miezi mitatu;

(c) lina sanduku la aluminiamu lenye mfuniko na limepakwa rangi nyeupe, mstari mwekundu na namba;

(d) halibebi kitu kingine tofauti na nyama.

Kuingiza mifugo katika machinjio

**15.**-(1) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kuhakikisha umiliki wa mfugo unaokusudiwa kuchinjwa unathibitishwa kabla ya kuingizwa katika eneo la machinjio.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakagua kibali cha usafirishaji wa mifugo na nyaraka nyingine zinazothibitisha umiliki.

(3) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atatunza rejista ya mifugo iliyopokelewa machinjioni ambayo itaainisha aina ya mifugo, jinsi, umri na taarifa za mmiliki.

Taratibu za kuingia machinjioni

**16.** Mtu yeyote anaetaka kuingia katika eneo la uzalishaji wa nyama anatakiwa kuomba kibali kwa

maandishi ndani ya saa sabini na mbili kabla ya siku ya kutembelea na meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio anaweza kumruhusu mtu huyo na kumtaka kuvaa mavazi maalumu yanayopatikana katika eneo la machinjio.

Ukaguzi wa mifugo

**17.-**(1) Mifugo inayokusudiwa kuchinjwa katika machinjio itafanyiwa ukaguzi wa awali na mkaguzi wa nyama kabla ya kuchinjwa.

(2) Endapo baada ya ukaguzi mifugo itagundulika kuwa na magonjwa hatarishi kwa afya ya binadamu au haijachanjwa, mifugo hiyo itahifadhiwa katika eneo maalumu kwa ajili ya matibabu.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuchukua kumbukumbu za mfugo aliyebainika kuwa na maradhi na za mmiliki na kumweka alama maalum itakayomtambulisha mfugo huo.

Sura ya 156

(4) Kabla ya mifugo kutengwa, taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama zitafuatwa.

(5) Endapo mifugo iliyotengwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) itaendelea kuwa na maradhi, Afisa Mwidhiniwa atamtaka mmiliki wa mifugo kuutoa nje ya eneo la machinjio kwa matibabu zaidi.

(6) Endapo mmiliki atashindwa kuondoa mifugo iliyotengwa ndani ya muda wa saa kumi na mbili tangu amri ya kuondolewa kwa mifugo itolewe, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru mifugo hiyo kuteketezwa kwa gharama ya mmiliki.

Uendeshaji wa shughuli za machinjioni

**18.-**(1) Meneja au mmiliki wa machinjio atahakikisha kuwa shughuli za machinjio zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za afya ikiwa ni pamoja na

(a) watoa huduma kupima afya kila baada ya miezi sita katika hospitali au kituo cha kutolea huduma za afya kwa kadri itakavyoelekezwa na Mkurugenzi;

(b) watoa huduma kuwa wasafi na kuvaa mavazi maalumu kwa ajili ya kazi hiyo;

(c) kutoruhusu mkusanyiko isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri;

(d) kuhakikisha kuwa eneo la machinjio linakuwa katika hali ya usafi wakati wote na kusimamia usafi wa jumla wa machinjio kila siku ya jumamosi ya mwisho wa mwezi;

(e) kutoruhusu kufanyika biashara nyingine yoyote katika eneo la machinjio.

(2) Mtu hataruhusiwa kuweka bucha, duka la nyama au biashara yoyote ya nyama ndani ya mita mia mbili kutoka eneo la machinjio.

(3) Mtu yeyote anayekusudia kuchinja mifugo atatakiwa kupeleka mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mifugo kwa madhumuni ya kuuza mahali pengine popote ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa.

(4) Nyama yoyote haitaruhusiwa kutumika kwa matumizi ya binadamu bila kufanyiwa ukaguzi wa mwisho na kuwa na muhuri maalum wa ukaguzi nyama.

(5) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza mifugo katika machinjio kwa ajili ya kuchinja baada ya saa kumi na moja kamili jioni isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Afisa Mwidhiniwa.

(6) Mtu yeyote hataruhusiwa kutoa nje ya eneo la machinjio mifugo hai, iliyokufa au nyama bila ya idhini ya maandishi ya meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio.

(7) Mtu hataruhusiwa kuchinja mifugo bila mifugo hiyo kufanyiwa ukaguzi wa awali.

Maradhi ya binadamu

**19**. Mtu anayejua kuwa anauguwa ugonjwa unaoambukiza kwa kugusana au kwa njia ya hewa au ana majeraha au michubuko hataruhusiwa kuingia katika eneo la machinjio au eneo la uzalishaji wa nyama isipokuwa kwa kibali cha daktari.

Ukaguzi wa nyama

**20.-**(1) Mkaguzi wa nyama atakuwa na wajibu wa kukagua nyama katika eneo la machinjio baada ya mifugo

kuchinjwa kwa madhumuni ya kubaini iwapo ubora wa nyama kwa matumizi ya binadamu.

(2) Endapo itabainika kuwa nyama iliyokaguliwa-

(a) inafaa kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi wa nyama atagonga nyama hiyo muhuri unaothibitisha kuwa nyama iliyokaguliwa ni salama kwa matumizi ya binadamu; au

(b) haifai kwa matumizi ya binadamu, nyama hiyo itateketezwa kwa kuchomwa moto au kwa njia nyingine itakayoonekana inafaa na mkaguzi atachukua kumbukumbu za nyama hiyo na za mmiliki wake.

(3) Endapo matokeo ya vipimo vya awali yatakuwa na mashaka kuhusu usalama wa nyama kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi wa nyama atahakikisha kuwa nyama husika inahifadhiwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne ili kuruhusu vipimo zaidi vya kimaabara kufanyika.

(4) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atatunza rejista ya nyama zilizokaguliwa ambayo itaonesha aina ya nyama, jinsi, umri, uzito na taarifa za mmiliki na kama nyama inafaa au haifai kwa matumizi ya binadamu.

Rejesta ya mifugo, nyama na mmiliki wa mifugo

**21.** Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kutunza rejesta ya mifugo, nyama na mmiliki wa mifugo ambayo inaonesha aina ya mfugo, jinsi, umri, uzito, jina na anuwani ya mmiliki wa mifugo.

Ada ya shughuli za machinjio

**22.** Halmashauri itatoza ada katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa kuhusiana na machinjio kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

Udhibiti wa ufugaji wa mbwa

**23.-**(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kufuga mbwa katika eneo la Halmashauri bila kibali cha ufugaji kutoka Halmashauri.

(2) Kibali cha ufugaji wa mbwa kitalipiwa kiasi cha shilingi elfu kumi na kitadumu kwa mwaka mmoja.

(3) Mfugaji wa mbwa atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuhakikisha mbwa anayemfuga anapata chanjo mbwa wake na analipa ada ya chanjo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;
(b) kuonesha cheti cha chanjo ya mbwa kabla ya kupata au kuhuisha kibali kilichoisha muda wake;
(c) kumfungia mbwa wake wakati wote wa mchana na anaweza kumfungulia kuanzia saa nne kamili usiku na kumfungia saa kumi na moja alfajir;
(d) kuogesha mbwa kila baada ya siku saba ili kudhibiti magonjwa na wadudu wasumbufu;
(e) kumfunga mbwa kwa mnyororo maalumu wakati wa kutembea naye kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa mujibu wa Sheria.

(4) Iwapo mfugaji atataka kusafirisha mbwa atalazimika kuwa na kasha maalum la kusafirishia mbwa kabla ya kupewa kibali.

(5) Halmashauri inaweza kumkamata na kumhifadhi kizuizini kwa muda usiozidi siku mbili mbwa anayezurura, na iwapo baada ya muda huo kupita hakuna mmiliki aliyetambulika, Halmashauri inaweza kuchukua hatua nyingine kadri itakavyofaa.

Kibali cha kutoa huduma za mifugo

**24.** Mtu anayekusudia kutoa huduma za mifugo kwa kuanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia vyakula vya mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga katika eneo la Halmashauri atalazimika kuwa na kibali maalumu kitakachoruhusu kutoa huduma hiyo kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Makosa

**25.** Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo-
(a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mifugo yake;
(b) atalisha mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) ataanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga bila utaalamu na bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri;
(d) atafuga mifugo bila kibali cha ufugaji;
(e) atashindwa au atazembea kutoa taarifa kuhusu uwepo wa ugonjwa wa mifugo katika banda lake;
(f) atauza, atalisha au atafunga mifugo pembezoni mwa barabara au sehemu ambayo haijaruhusiwa;
(g) atasababisha kero au chukizo kwa jamii;
(h) ataruhusu mifugo yake kuzurura ovyo;
(i) atashindwa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mfugo au mifugo yake;
(j) ataingia katika eneo la machinjio akiwa amelewa au atatumia au kuingiza kilevi katika eneo la machinjio;
(k) atatumia lugha za kashfa, kuudhi, kudhalilisha au matusi ndani ya machinjio au kufanya udhalilishaji wa aina yoyote;
(l) atabandika au kubandua tangazo lolote bila idhini ya meneja au mmiliki wa machinjio;
(m) atahatarisha amani au kushiriki kwa namna yeyote kuhatarisha amani katika eneo la machinjio;
(n) atafanya au kushiriki kufanya uchafuzi wa mazingira;
(o) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

**26.** Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa kinyume na Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Kufifilisha kosa

**27.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya

Sheria Ndogo hii kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii na kulipa ada anayodaiwa.

Kufutwa kwa TS Na. 533 la 2019

**28.** Sheria Ndogo za Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2019 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(4))*

IDADI YA MIFUGO ILIYORUHUSIWA KUFUGWA

| Na. | Aina ya Mifugo | Idadi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero au chukizo kwa jamii |
| 2. | Mbuzi au kondoo | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero au chukizo kwa jamii |
| 3. | Nguruwe | 4 | Nguruwe watoto wakiachishwa kunyonya wauzwe au kuondolewa |
| 4. | Mbwa | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero au chukizo kwa jamii |
| 5. | Wanyama wa jamii ya ndege | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero au chukizo kwa jamii |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

KIBALI CHA KUFUGA MIFUGO

Jina la Mfugaji:………………………………………………………..
Anuani:………………Nama ya simu…………………………...........
Kata:…………………………………… Mtaa ……………………........
Namba ya nyumba:………………………… Namba ya kitalu:……………
Ameruhusiwa kufuga Mifugo ifuatao katika eneo la…........…...........……..

| Na. | Aina ya Mfugo | Koo | Idadi ya Mifugo | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jike | Dume | |
| 1 | Ng'ombe | | | | |
| 2 | Mbuzi | | | | |
| 3 | Kondoo | | | | |
| 4 | Nguruwe | | | | |
| 5 | Ngamia | | | | |
| 6 | Punda | | | | |
| 7 | Paka | | | | |
| 8 | Farasi | | | | |
| 9 | Sungura | | | | |
| 10 | Mbwa | | | | |
| 11 | Kuku au Bata | | | | |
| 12 | Wanyama wengine ambao hawakutajwa | | | | |

*Tangazo la Serikali Na.43 (Linaendelea.)*

Kibali hiki kimetolewa kwa Ndugu: ………………………………………kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kwa mifugo kuanzia tarehe……………..hadi tarehe……………

Kimetolewa na:
Jina la Afisa Mwidhiniwa………………………………..Saini………
Wadhifa:……………………………………………………………..
Tarehe:…………………
Muhuri:……………………………………………

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8(1))*

### KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO

Jina:…………………………………………….
Anuani:…………………………………………
Ameruhusiwa kusafirisha mifugo ifuatayo kutoka ………………kupitia njia za……….......hadi…………..…..

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi ya Mifugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | |
| 2. | Mbuzi | |
| 3. | Kondoo | |
| 4. | Nguruwe | |
| 5. | Ngamia | |
| 6. | Punda | |
| 7. | Paka | |
| 8. | Farasi | |
| 9. | Sungura | |
| 10. | Mbwa | |
| 11. | Kuku au Bata | |
| 12. | Mifugo mingine ambayo haikutajwa | |

Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku…..... kuanzia tarehe…........hadi tarehe……….
Kimetolewa na :
Jina la Afisa Mwidhiniwa:……………………………………….
Saini:…………………………………………………………..
Wadhifa:………………………………………………………
Tarehe:………………………………………………………..
Muhuri:……………………………………............................

## JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22)*

### ADA KWA AJILI YA SHUGHULI ZA MACHINJIONI

A. Ada ya ukaguzi wa nyama katika machinjio

| Na. | Aina ya mnyama | Aina ya machinjio | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kijiwe cha kuchinjia (slaughter slab) | Nyumba ya kuchinjia (slaughter house) | Machinjio ya kisasa (Abattoir) | |
| | | | | Matumizi ndani ya nchi | Matumizi nje ya nchi |
| 1 | Kwa kila ng'ombe | 4,000 | 5,000 | 15,000 | 20,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Kwa kila mbuzi au kondoo | 1,000 | 2,500 | 5,000 | 10,000 |
| 3 | Kwa kila nguruwe | 2,000 | 4,000 | 5,000 | 10,000 |
| 4 | Kwa kila kuku | 500 | 500 | 1,000 | 1,500 |

B. Ada za huduma ya Machinjio

B1. Soko la ndani au nje (kupoza nyama)

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kupoza nyama ya ng'ombe mmoja chini ya saa 24 | 15,000 kwa kila siku |
| 2 | Ada ya kupoza nyama ya ng'ombe mmoja baada ya saa 24 | 20,000 kwa kila siku |
| 3 | Ada ya kupoza nyama ya mbuzi na kondoo mmoja chini ya saa 24 | 10,000 kwa kila siku |
| 4 | Ada ya kupoza nyama ya mbuzi na kondoo mmoja baada ya saa 24 | 15,000 kwa kila siku |

B2. Soko la ndani au nje (kugandisha nyama)

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kugandisha nyama nyama ya ng'ombe mmoja | 20,000 kwa kila siku |
| 2 | Ada ya kugandisha nyama nyama ya mbuzi na kondoo mmoja | 15,000 kwa kila siku |

B3. Kulipua nyama (blasting) ya ng'ombe, mbuzi na kondoo

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kulipua nyama ya ng'ombe mmoja | 10,000 kwa masaa 12 |
| 2 | Ada ya kulipua nyama ya mbuzi na kondoo mmoja | 5,000 kwa masaa 12 |

B4. Soko la ndani na nje (kupoza mazao mengine ya nyama)

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kupoza mazao ya nyama ya ng'ombe mmoja chini ya masaa 12 | 5,000 kwa kila siku |
| 2 | Ada ya kupoza mazao ya nyama ya ng'ombe mmoja baada ya masaa 12 | 5,000 kwa kila siku |
| 3 | Ada ya kupoza mazao ya nyama ya mbuzi na kondoo mmoja chini ya masaa 12 | 2,500 kwa kila siku |
| 4 | Ada ya kupoza mazao ya nyama ya mbuzi na kondoo mmoja baada ya masaa 12 | 2,500 kwa kila siku |

C. Ada nyingine za huduma za machinjio na mabucha

| Na. | Aina ya chanzo | | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya kutunza ng'ombe mmoja katika machinjio | | 10,000 kwa siku moja |
| 2 | Ada ya kutunza mbuzi au kondoo mmoja katika machinjio | | 5,000 kwa siku moja |
| 3 | Ada ya kusafirisha nyama kwa gari | chini ya tani moja | 6,000 kwa safari |
| | | tani 1 hadi 5 | 8,000 kwa safari |
| | | zaidi ya tani 5 | 10,000 kwa safari |
| 4 | Ada ya pikipiki inayobeba nyama (mabuchani) | | 1,000 kila safari |
| 5 | Ada ya damu mbichi (isiyo na maji) katika machinjio | | 10,000 – 15,000 kwa kila pipa moja |
| 6 | Ada ya damu iliyokaushwa | | 2,000 kwa kilo moja |
| 7 | Ada ya matumbo | kwa ng'ombe | 500 kwa kila tumbo moja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kwa mbuzi au kondoo | 200 kwa kila tumbo moja |
| 9 | Ada ya kichwa | cha ng'ombe | 500 kwa kila kichwa |
| | | cha mbuzi au kondoo | 200 kwa kila kichwa |
| 10 | Ada ya miguu ya ng'ombe, mapafu, maini, ulimi na mazao mengine | | 1000 |
| 11 | Ada ya kutumia bucha la Halmashauri kwa nondo moja | kwa ng'ombe | 1000 kwa siku |
| | | kwa mbuzi na kondoo | 500 kwa siku |
| 12 | Ada ya masalia ya nyama (vyakula vya mbwa) katika machinjio | | 5000/= kwa kilo |
| 14 | Ada ya nyongo katika machinjio | | 2,000 kwa kila lita moja |
| 15 | Ada ya pembe, kwato na mfupa ya ng'ombe, mbuzi na kondoo | | 100 kwa kilo |
| 16 | Ada ya mbolea (Organic Manure) katika machinjio | | 50,000 kwa lori moja |
| 17 | Ada ya jiwe la nyongo (Gallstones) kwa gramu moja (mwenye ng'ombe atajulishwa) | | 50,000 |
| 18 | Ada ya mazagazaga (vitabu, mikia, via vya uzazi na mengine) | | 500 |
| 19 | Mkojo (animal urine) kwa lita | | 100 |
| 20 | Ada ya gari la kubeba mifugo (parking) | chini ya tani 7 | 5,000 |
| | | kuanzia tani 7 mpaka 10 | 10,000 |
| | | zaidi ya tani 10 | 15,000 |

D. Ada za huduma nyingine za mifugo

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya huduma za ndani kliniki ya mifugo | 5,000 |
| 2 | Ada ya huduma za nje kliniki ya mifugo | 10,000 |
| 3 | Ada ya uhamilishaji kwa kila ng'ombe au nguruwe mmoja | kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Serikali |
| 4 | Ada ya chanjo za mifugo | kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Serikali |
| 5 | Ada ya utambuzi, uandikishaji na usajili wa mifugo (uvalishaji hereni) | kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Serikali |

E. Ada za leseni za eneo, uchunaji wa ngozi na upangaji madaraja

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi (kwa shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya leseni ya uchunaji | 10,000 kwa mwaka |
| 2 | Ada ya maombi ya leseni ya uchanaji | 5,000 kila ombi |
| 3 | Ada ya leseni ya upangaji wa madaraja ya ngozi | 10,000 kwa mwaka |
| 4 | Ada ya maombi ya leseni ya kupanga madaraja | 5,000 kila ombi |
| 5 | Ada ya leseni ya banda la kukaushia ngozi | 10,000 kwa mwaka |
| 6 | Ada ya fomu ya maombi ya leseni ya banda la kukaushia ngozi | 20,000 kwa fomu |
| 7 | Ukaguzi wa afya | 40,000 kwa mwaka |
| 8 | Usajili wa vikundi vinavyojihusisha na zao la ngozi | 100,000 kwa mwaka |
| 9 | Leseni ya ghala la kuhifadhia ngozi zaidi ya 500 | 100,000 kwa mwaka |
| 10 | Leseni ya ghala la kuhifadhia ngozi 100 - 500 | 50,000 kwa mwaka |
| 11 | Leseni ya ghala la kuhifadhia ngozi chini ya 500 | 10,000 kwa mwaka |
| 12 | i. Kuuza ngozi mbichi kwa wakusanyaji (machinjioni) | 100 kwa kipande |
| | ii. Kuuza ngozi zenye chumvi (wasindikaji) | 200 kwa kipande |
| 13 | i. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa zaidi ya tani 5 | 150,000 kwa safari |

| | | |
|---|---|---|
| | ii. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa tani 1 hadi tani 5 | 100,000 kwa safari |
| | iii. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa chinii ya tani 1 | 25,000 kwa safari |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ………. Mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni …… ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, NINAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi ............................................ kama faini ya ufifilishaji wa kosa na kiasi cha shilingi ...................... cha ushuru au ada ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YA MKURUGENZI:
Jina:…………………………………..……………………
Saini: ………………………….………………………….….
Tarehe………………………………………………….…

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,
*Mkurugenzi wa Jiji,*
*Halmashauri ya Jiji,*
*Dasr es Salaam*

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,
*Mstahiki Meya,*
*Halmashauri ya Mji,*
*Handeni*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*